TANZANIA COFFEE ASSOCIATION

MADA:Nafasi ya Sekta Binafsi Katika KuongezaTija Kwenye Sekta ya Kahawa.

Maana ya Sekta binafsi

- Sekta binafsi- ni sekta inayojumuisha sekta zote ambazo sio taasisi za umma(PPP Act,2010).
- Sekta ya Umma- Sekta ya umma inajumuisha serikali kuu, serikali za mitaa na taasisi zote zinazofanya kazi kwa niaba ya serikali kuu.

Nafasi ya TCA kwenye Sekta ya kahawa

- Kuwaunganisha wadau binafsi wote kwenye sekta ya kahawa na kuwa na sauti moja dhidi ya mambo yanayoathiri sekta ya kahawa.
- Kulinda na kutetea maslai ya wadau wa sekta binafsi katika sekta ya kahawa.
- Kutoa taarifa mbalimbali zinzoahusu sekta ya kahawa kwa wanachama ili kuboresha mnyororo wa dhamani.

Sekta binafsi kwenye kahawa

1. Makampuni yauzayo kahawa nje.
2. Vyama vya ushirika.
3. Taasisi za kifedha.
4. Mashirika yasiyo ya kiserikali(Makundi ya kutoa huduma).
5. Viwanda vya kukobolea, kukaanga, kuchakata
6. Wanunuzi binafsi.
7. Taasisi za utafiti.
8. Mkulima.

Mahusiano ya wadau wa kahawa na mkulima



Mchanganuo wa uhusiano wa sekta binafsi na mkulima

1. Kuongeza uzalishaji
2. Upatikanaji wa huduma za kifedha
3. Kuwaunganisha wakulima na masoko-hasa Soko la nje
4. Ukoboaji wa kahawa ya mkulima.

1.Kuongeza uzalishaji

- Miche bora ya kahawa (Taasisi za utafiti)

2.Upatikanaji wa Mitaji kwa wakulima

- Mabenki- taasisi za kifedha zimeweka huduma ya stakabadhi ghalani hivyo kumsaidia mkulima kuweza kukusanya kahawa.
- Makampuni- baadhi ya vyama vya wakulima vimepewa mikataba wanayoweza kuitumia kama dhamana kupata fedha kutoka taasisi za fedha ndani na nje ya nchi.

3.Huduma mbalimbali kwa mkulima

- Mtaala wa kahawa utasaidia wakulima kuijua vizuri sekta na nafasi yao kwenye mnyororo wa thamani (Ushirikiano wa sekta binafsi na serikali ukiongozwa na TCB kwa ushirikiano na IDH,Washirika binafsi 6 wa CPT,Yara Ltd na Café Africa.
- Mafunzo kwa wakulima. Mfano;Utunzaji bora wa mahesabu ,jinsi ya kuongeza ubora kwa kuzingatia njia bora za kuandaa kahawa kwenye CPU.
- Teknolojia.Mfano,RITS (Relation Information Tracking System) - kumsaidia mkulima kufuatilia ukusanyaji na kutoa kutoa taarifa sahihi kwenye masoko.

4.Ukoboaji wa kahawa

- Kwa sasa kila kanda kuna viwanda vya kukobolea kahawa. Hii imesaidia
    i. Kupunguza gharama za usafirishaji.
    ii. Kuleta unafuu kwenye bajeti ya mkulima.
    iii. Kuepukana na hatari za wizi barabarani.
    iv. Kulinda ubora.

Namna ya kuongeza mapato kwa mkulima.

Hapa kunaitajika nguvu ya pamoja baina ya serikali na sekta binafsi katika maeneo ambayo bado kuna changamoto;

- Wakulima na wadau wengine kuendelea kujiunga na TCA.

kwa pamoja kujenga sauti moja juu ya mambo yanayogusa sekta.

a) Kodi

b) leseni

c)Ushuru

Namna ya kuendelea kuongeza mapato kwa mkulima,inaendelea.....

- Ushiriki wa serikali katika kuweka mazingira bora kwenye sekta ya kahawa.
- Halmashauri kutenga bajeti kwa ajili ya kuendeleza zao la kahawa
- Wadau binafsi wana wajibu wa kumhakikishia mkulima bei inayokidhi gharama ya uzalishaji na faida kwa kazi yake.

Matarajio katika sekta ya kahawa

- ICO inakadiria mahitaji ya kahawa duniani kufikia magunia milioni 175.8 ifikapo 2020.

  -2014/15 uzalishaji :magunia milioni 144
- Upungufu unaokadiriwa ni magunia 30 milioni.
- Tanzania tuna nafasi ya kuweza kuongeza uzalishaji na kufidia nakisi inayokadiriwa.

Hitimisho

- Bado zipo faida za kutosha za kuendeleza uhusiano kati ya sekta binafsi na wakulima wadogo.
- Sekta binafsi haiwezi kufanikiwa yenyewe,serikali haiwezi kufanikiwa yenyewe hivyo ni lazima kuwe na ushirikiano kati ya serikali na sekta binafsi kwa faida ya mkulima mdogo.

Ahsanteni.